# MAHAKAMANI

## Mama azua majonzi kortini

Na NICHOLAS NGOLYO

Mama mmoja jana alifanya watu katika Mahakama ya Kibera walie machozi aliposimulia alivyoshikwa na kushtakiwa kwa kudai chakula.

Shukri Gaabou Adan, alisema alifungiwa katika Kituo cha Polisi cha Kilimani kwa siku nne pamoja na watoto wake wawili wadogo bila kupewa chakula.

"Mimi ni mdhaifu sana kutokana na njaa na pia nimedungwa sindano," Bi Adan akasema. Baadhi ya watu walionekana wakipanguza machozi kwa vitambaa kutokana na mateso ambayo mama huyo alisema alipitia kabla ya kufikishwa mahakamani.

Mahakama ya Hakimu Mwandamizi, Catherine Mwangi, ilifurika kwa watu, wakiwemo mawakili ambao walionyesha masikitiko yao kutokana na maelezo ya mwanamke huyo mkimbizi kutoka Somalia.

Wakili, Cecil Miller, alijitolea kumnunulia mshtakiwa na watoto wake chakula. Hakimu alishangazwa na shtaka lililowasilishwa mahakamani akisema haiwezekani kwa mtu kushtakiwa kwa kudai.

"Mshtakiwa alidai chakula kutoka kwa afisa wa shirika la UNHCR na haikuwa vyema kumshtaki. Shtaka halisemi aliharibu mali wala kutusi afisa huyo ila linasema alimpigia kelele tu," Bi Mwangi akasema.

"Unataka tuchukue watoto wako tumpe huyu wakili (Bw Miller) awatunze na wewe urudishwe katika kambi ya wakimbizi," Bi Mwangi alimuuliza mshtakiwa.

"Siwezi kuachia mtu mwingine watoto wangu. Heri nife nao tu," mshtakiwa akasema.

Alisema mumewe alitoroka watu walipokuwa wakiuawa Somalia na kumuacha na watoto. Aliomba apelekwe katika kambi ya wakimbizi ya Daadab badala ya kurudishwa Somalia. Hakimu aliagiza mshtakiwa apelekwe Daadab.

## Alivyojeruhi afungwa

ASHTAKIWA KUTUMIA HATI BANDIA



## Ashtakiwa kwa kuibia Shirika la Reli Kenya

Na MARTIN OCHOLA

Mtu ambaye aliiba mali ya Shirika la Kenya Reli jana alifikishwa katika mahakama ya Makadara, mjini Nairobi.

Peter Magendo Njoroge alikiri mashtaka mbele ya Hakimu Mkuu wa Makadara, Bw Muga Apondi.

Ingawa mshtakiwa alikiri shtaka lake, Bw Apondi aliagiza ripoti yake ya hapo awali kutoka kwa afisa wa Probesheni mnamo Juni 4 kabla ya kutoa uamuzi wake.

Shtaka lilisema mnamo Mei 20, mwaka huu, katika Kituo cha Reli cha Dagoreti, mshtakiwa, akishirikiana na wengine ambao hawakuwa mahakamani, aliiba vipuri vya gari vitatu vya thamani vya Sh6,000.

Kiongozi wa mashtaka, Inspekta Mkuu Michael Mukui, aliambia mahakama kuwa, siku hiyo, mwendo wa saa 12 asubuhi, mlinzi wa Shirika la Reli alimuona mshtakiwa akitembea kwenye kiwanja hicho akiwa na wasiwasi, huku akibeba mfuko.

Aliposimamishwa, mshtakiwa alitupa mfuko chini na kutimua mbio. Lakini alishikwa muda mfupi baadaye na kupelekwa katika Kituo cha Polisi ambako